# Mwongozo wa Mpango Kupimwa na Kuwa Shuleni wa FCPS

Shule za Umma za Kata ya Fayette zimejitolea kutoa mafundisho ya kibinafsi wakati wa mwaka wa shule 2021-22 na imetekeleza mikakati ya kuzuia yenye ngazi tofauti iliyopendekezwa na wataalam wa afya na matibabu ili kuhakikisha mazingira salama ya kujifunzia kwa wanafunzi na mahali salama pa kazi kwa walimu na wafanyakazi.

Mtindo Delta wa COVID-19 inatawanyika kwa urahisi na haraka sana, hata kwa kufuata hatua kali za usalama za wilaya. Kwa kuwa shule zinaonyesha jamii tunamohudumia, viwango vya sasa vya virusi katika Kata ya Fayette vimesababisha visa vya COVID-19 katika shule hadi ku karantini.

Katika hatua za kupunguza kiwango cha muda wa kufundishwa ambao wanafunzi wanapoteza wakati wamewekwa karantini, FCPS inarekebisha itifaki zake za karantini na kujaribu mpango wa "Kupimwa na Kukaa" kwa kushirikiana na Idara ya Afya ya Kata ya Lexington-Fayette na Vituo vya Amerika vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC). Hii itifaki ya jibu la kupima na ku karantini imeonekana kwa kawaida kuwa kama vile ku karantini kwa mawasiliano ya shule na ni njia nyingine ya usalama kuliko kutengwa nyumbani.

## Sehemu ya 1: Nani anaweza kujitenga?

Wanafunzi ambao walipimwa na kupatikana na COVID-19 wanahitajika kujitenga kwa kiwango kisicho chini ya siku 10 baada ya dalili za kwanza au, ikiwa hawana dalili, baada ya kupata matokeo ya vipimo inayoonyesha kama wana virusi.

Wanaweza kurudi shuleni baada ya siku 10, na fomu ya kutolewa kitengo kutoka Idara ya Afya ya Kaunti ya Lexington-Fayette au daktari, IKIWA wamekuwa na dalili bure kwa masaa 24 bila kuchukua dawa za kupunguza dalili.




NA



## Sehemu ya 2: Mawasiliano ya karibu ni nini?

Mawasiliano ya karibu" kwa wanafunzi hufafanuliwa kama:

Chini ya futi 3



Kuwa ndani ya futi 3 au chini, darasani, na ikiwa watu wote wawili wamevaa barakoa.

**AU**

Chini ya futi 6



Kuwa ndani ya futi 6 au chini, kwa jumla ya muda wa dakika 15, siku ya shule, ikiwa moja au watu wawili hawavae barakoa.

## Sehemu ya 3: Kujitenga

**<u>Wanafunzi waliotambuliwa kuwa na "mawasiliano ya karibu" na mtu ambaye aliyepimwa na kuonekana kuwa na COVID-19, wakiwa wanaambukiza, wanawekwa kitengoni.</u>**

**<u>Isipokuwa:</u>**

- ***Hawana dalili, wana chanjo kamili, na mawasilano ya karibu:*** Wanafunzi ambao wamepewa chanjo na hawapati dalili za COVID-19 hawaitaji kupimwa na itifaki ya majibu ya karantini. Ila ijapokuwa hawata karantini, lazima wachunguze dalili hadi siku 14 na wapimwe ikiwa wanaonyesha dalili. Na ikiwa wanaanza kuwa na dalili za COVID-19, wakati wote mnamo siku 14 za kutengwa, wanafunzi wanapaswa kufuata mahitaji yaliyoainishwa katika Sehemu ya 5: Itifaki za Karantini kwa Wanafunzi WENYE Dalili za COVID-19. Ikiwa wana dalili au la, bado inashauriwa kuwa watu hawa wapimwe COVID-19 mnamo siku tatu na tano ya mawasiliano.
- ***Wawasiliani wa karibu ambao waligonjwa COVID-19 mnamo siku 90 zilizopita:*** Watu ambao wametambuliwa kuwa na COVID-19 mnamo siku 90 kabla ya mawasiliano hawastahili kupimo na itifaki za majibu ya karantini ikiwa.




Mawasiliano ilitokea ndani ya siku 90 tangu mwanzo wa ugonjwa wao.

**NA**



Mtu aliyewasiliana amepona na amebaki bila dalili za COVID-19.

# Sehemu ya 4: Itifaki za kujitenga kwa Wanafunzi WASIYO na dalili za COVID-19

Wanafunzi waliowekwa kwenye karantini kwa sababu ya mahambukizi shuleni na ambao hawana dalili, lazima wafuate moja ya itifaki hizi tatu. Ila, ni kwa kila familia kuamua ni itifaki gani wanayotaka watoto wao wafuate. Katika chaguo zote tatu, ni lazima familia ziendelee kufuatilia dalili za mtoto wao kwa siku 14 (siku ya kwanza ya mawasiliano huhesabiwa kama siku 0). Ikiwa wanaanza kuwa na dalili za COVID-19 wakati wowote mnamo siku 14, wanafunzi wanapaswa kufuata tahadhari iliyolainishwa katika Sehemu ya 5: Itifaki za Kutengwa kwa Wanafunzi WENYE Dalili za COVID-19.

## Itifaki A: Kujitenga Nyumbani




Kukaa nyumbani mbali ya shule kwa muda wa siku 10 za kalenda tangu siku ya mawsiliano. (Siku ya mawasiliano ikiwa kama siku 0.)

→



Kufuatilia dalili za COVID-19

→



Kurudi shuleni siku ya 11, maadamu hawaoni dalili za COVID-19

## Itifaki B: Kupimwa na Kufupisha Karantini




Kukaa nyumbani, mbali ya shule kwa siku 7. (Siku ya mawasiliano ikiwa kama siku 0.)

→



Kufuatilia dalili za COVID-19

→




Kupimwa COVID-19 siku ya 5 AU siku ya 6 AU siku ya 7

→



Ikiwa matokeo ya kipimo iko hasi, rudi shuleni siku ya 8, mahadamu hakuna dalili za COVID-19

## Itifaki C: Kupimwa na Kubaki Shuleni

*Kumbuka: Itifaki C inapatikana tu kwa wanafunzi waliotengwa kwa sababu ya mawasiliano shuleni. Wanafunzi walio na mawasiliano ya karibu ya mgonjwa nyumbani au nje ya shule lazima wafuate Itifaki A au B.*



Kufuatilia dalili za COVID-19

→



Kuja shuleni kila asubuhi ilimradi hawapati dalili zozote za COVID-19

→



Kupimwa COVID-19 shuleni kila Jumatatu, Jumatano na Ijumaa hadi siku 7 baada ya mawasiliano na mgonjwa. * (Siku ya mawasiliani ikiwa ni siku 0.)

↗



Ikiwa kipimo iko hasi, baki shuleni. Wanafunzi wanapaswa kujiepusha na shughuli zingine, isipokuwa shughuli za shule, hadi siku ya 8.

**AU**

↘



Ikiwa kipimo ni kamilifu, nenda nyumbani na ufuate mahitaji ya kutengwa kwa kesi ya COVID-19.

*(Kumbuka: ikiwa kipindi cha siku 7 kutoka tarehe ya kuwasiliana na mgonjwa ni wikendi au siku ya likizo, yaani wakati shule imefungwa, watu wataendelea kujitenga nyumbani na baadaye wanapimwa COVID-19 siku inayofuata ya kipimo shuleni.)*

# Sehemu ya 5: Itifaki za kujitenga kwa Wanafunzi WENYE dalili za COVID-19

Wanafunzi waliowekwa kwenye karantini ambao wanaonyesha dalili za COVID-19 mnamo siku 14 tangu siku ya mawasiliano yao ma mgonjwa, ni lazima wakae nyumbani, wasije shuleni na wafuate moja ya itifaki hizi mbili.  Walakini, ni jukumu la kila familia kuamua ni itifaki gani ambayo wanataka watoto wao wafuate.

## Itifaki D: Jipimishe

Familia zinaweza kuchagua watoto wao wapimwe COVID-19 wakati wanaonyesha dalili, na:



Ikiwa matokeo ya vipimo inakamilisha COVID-19, fuata itifaki za kujitenga.

Piga simu 859-381-3277 (FCPS) kuripoti kesi kamilifu.

**AU**



Ikiwa matokeo ya vipimo haionyeshe COVID-19, tafuta utambuzi mwengine kutoka kwa mtoa huduma ya msingi NA fuata maagizo ya kurudi shuleni kutoka kwa daktari huyo.

*Kumbuka: Ikiwa ameelekezwa na daktari arudi shule kabla ya kumalizika kwa kipindi cha karantini cha awali, endelea na utimize itifaki ya "karantini nyumbani," au "Pimwa kwa kufupisha," au "Kupimwa na Kukaa."*

## Itifaki E: Hakuna Kipimo

Ikiwa familia zinahamua watoto wao KUTO fanya vipimo vya COVID-19:




Kaa nyumbani, mbali ya shule, kwa siku 10 za kalenda.

**NA**




Rudi shuleni ikiwa hakuna dalili kwa masaa 24 bila kutumia dawa za kupunguza dalili.